

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya ileje Bi. Nuru Waziri Kindamba ametoa rai kwa Wasimamizi wa Mikopo ngazi ya Kata katika wilaya hii , kuwahimiza vikundi vya Vijana , wanawake na Wenye Ulemavu kujitokeza kukopa mikopo ya asilimia kumi inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli za maendeleo.

Bi. Kindamba ametoa rai hiyo wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wasimamizi wa Mikopo ambao ni Maafisa Maendeleo ngazi ya Kata katika wilaya hii,yaliyofanyika katika ukumbi wa Halmashauri, ambapo amewahimiza wasimamizi hao kutoa mikopo kwa walengwa husika ili kuwanufaisha katika shughuli za maendeleo.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji, amewataka wasimamizi hao kuwakumbusha walengwa wa mikopo hiyo kuilipa ndani ya muda husika ili iweze kuwanufaisha na walengwa wengine. sambamba na kuitumia mikopo hiyo vizuri kwa shughuli husika ya maendeleo.

Sambamba na hayo Bi, Kindamba ametoa rai kwa wasimamizi wa mikopo kuepuka mianya ya ubadhirifu katika zoezi zima la kutoa mikopo hiyo kwa walengwa, Katika halimashauri ya wilaya ya Ileje jumla ya shilingi 626,768,909.01 zimetengwa kwa ajili ya kukopesha vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu.